TANGAZO LA SERIKALI NA. 905 la tarehe 22/12/2023

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 6(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMSHAURI YA WILAYA YA MLIMBA YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmshauri ya Wilaya ya Mlimba ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmshauri ya Wilaya ya Mlimba.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"afisa mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmshauri ya Wilaya ya Mlimba;

"kibali" maana yake ni idhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"mhudumu" maana yake ni mtu anayehudumia wateja katika baa, hoteli, mgahawa, mama lishe au baba lishe;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"soko" maana yake ni eneo au soko lililotengwa na linalomikiwa na Halmashauri kama soko;

"stendi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo hii itajumuisha pia kituo cha kupaki malori na vituo vingine vidogo vidogo vya kupakia na kushusha abiria vya Halmashauri;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri; na

"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada na ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo ya (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hii zitalipwa kwa Halmashauri.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

5. Mtu anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii

Muda wa kukusanya ada na ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada na ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri au wakala kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

Utoaji wa stakabadhi za malipo

7.-(1) Ada au ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, utalipwa kwa Halmashauri au kwa Wakala ambaye atatoa stakabadhi ya kielektroniki kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

(2) Utakuwa ni wajibu wa kila mlipa ada au ushuru kudai na kuhakiki stakabadhi ya malipo kulingana na kiasi cha fedha alicholipa.

(3)Utakuwa sio utetezi chini ya Sheria Ndogo hii mtu kudai kuwa amelipa ada au ushuru lakini hakupewa stakabadhi ya kielektroniki.

Ukusanyaji wa madeni

8.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za wadaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Halmashauri baada ya kupata idhini ya Mahakama itakuwa na mamlaka ya kuuza mali za mdaiwa kwa njia ya mnada baada ya siku thelathini kupita tangu

kukamatwa kwa mali za mdaiwa.

(4) Halmashauri baada ya kupata kibali cha Mahakama itakuwa na uwezo wa kuuza mali zilizokamatwa ambazo zinaweza kuharibika kwa haraka kabla hazijaharibika

(5) Bila kuathiri masharti ya aya hii, kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Halmashauri itatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala

Ushuru wa nyumba za kulala wageni

9.-(1) Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni anapaswa kulipa asilimia kumi ya mapato yaliyolipwa na mgeni aliyesajiliwa.

(2) Mmiliki wa nyumba ya kulala wageni atawajibika kuwasilisha ushuru wa nyumba ya kulala wageni kila mwezi kwa Halmashauri ndani ya siku saba tangu kumalizika kwa mwezi wa malipo.

Uteuzi wa wakala

10. -(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya

11. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, afisa

afisa mwidhiniwa

mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii

Ulipaji wa gharama za kuhifadhi mzigo au chombo kilichokamatwa

12.-(1) Halmashauri itatoza kiasi cha asilimia tano ya thamani ya chombo kilichobeba mzigo kwa kila siku kwa mzigo ulioshikiliwa baada ya kukamatwa ukisafirishwa bila ya kulipa ada au ushuru.

(2) Chombo au mzigo husika usipokuwa umelipiwa kwa muda wa siku saba Halmashauri itauza mzigo au chombo hicho kwa njia ya mnada ili kufidia gharama zake.

Fidia ya gharama za uendeshaji wa zoezi.

13. Endapo anayetakiwa kulipa ada au ushuru atakwepa kulipa, gharama zote ambazo zitakuwa zimetumika na Halmashauri wakati wa kumkamata, mkosaji atawajibika kuzilipa.

Makosa na adhabu

14.-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;
(c) atamzuia Mkurugenzi au afisa mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ushuru na zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri; au
(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu, au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;

(f) atashindwa, atadharau, atakaidi au kukataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii;

(g) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri; au

(h) atatumia chombo chochote kusafirishia bidhaa ambayo haijalipiwa ushuru au ada.

(2) Mtu atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti yoyote katika Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

15. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengezwa chini ya aya ya 4(1))*

SEHEMU YA KWANZA: USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Namba. | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mchanga au kokoto za mawe | 2,500/= kwa mita moja ya ujazo |
| 2. | Kibali cha kuchimba madini ya ujenzi | Hakuna |
| 3. | Kifusi | Hakuna |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Kibali cha kufyatua tofali za udongo au kuchoma tanuru | 5,000/= kuanzia matofali 10,000 kwa mwaka. |

SEHEMU YA PILI: ADA YA KUKODI MALI ZA HALMASHAURI NA VIFAA VYA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya kifaa | Kiwango cha ada au ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | (i) Kumbi za Halmashauri.<br>(a)Ukumbi mkubwa<br>(b)Ukumbi mdogo | (a)500,000/= kwa siku moja<br>(b) 200,000/= kwa siku moja |
| 2. | (ii) Viti vidogo<br>(iii) Viti vya chuma | 200/=kwa kimoja kwa siku<br>300/= kwa kimoja kwa siku |
| 3. | Meza ndogo | 300/= kwa kimoja kwa siku moja |
| 4. | Meza kubwa | 500/= kwa kimoja kwa siku moja |
| 5. | Vibanda vya Halmashauri kuzunguka stendi kuu | Kwa mujibu wa mkataba |
| 6. | Vibanda vya biashara sokoni | Kwa mujibu wa mkataba |
| 7. | Majengo mengine ya Halmashauri | Kwa mujibu wa mkataba |

SEHEMU YA TATU: USHURU WA UKAGUZI WA NYAMA

| Namba. | Aina ya mfugo | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 3000/= kwa siku |
| 2. | Mbuzi au kondoo | 1000/= kwa siku |
| 3. | Nguruwe | 2000/= kwa siku |

SEHEMU YA NNE:USHURU YA UTUMIAJI WA SOKO

| Namba | Aina ya bidhaa | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | meza | 300/=kwa siku |

SEHEMU YA TANO: USHURU WA MINADA AU MAGULIO KWA WASIO NA VITAMBULISHO VYA WAJASILIAMALI WADOGO

| Namba. | Aina ya Bidhaa | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 4,000/= kwa kila mmoja |
| 2. | Kondoo | 1000/= kwa kila mmoja |
| 3. | Mbuzi | 1000/= kwa kila mmoja |
| 4. | Wanyama aina nyingine | 1,000/= kwa kila mmoja |
| 5. | Bidhaa zinazotengenezwa viwandani au karakana | 1000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Wauza mitumba | 1000/= |
| 7. | Wauza pombe za kisasa na vinywaji baridi | 1,000/= |
| 8. | Wauza nafaka | 1000/= kwa kila gunia |
| 9. | Mifugo jamii ya ndege | 1000/= kwa tenga |
| 10. | Pombe za asili | 1000/= |
| 11. | Wauza dawa za asili | 1000/= |
| 12. | Wauza vipuri vya baiskeli au pikipiki au magari | 1000/= |
| 13. | Wauza dagaa | 1000/= |
| 14. | Wauza samaki | 1000/= |
| 15. | Wauza chumvi,nyama na mboga za majani | 1000/= |
| 16. | Wauza vyungu | 1000/= |
| 17. | Wauza vyombo vya nyumbani | 1000/= |
| 18. | Wauza viatu | 1000/= |
| 19. | Wauza nguo mpya | 1000/= |
| 20. | Mafundi baiskeli | 1000/= |
| 21. | Bidhaa nyingine ambazo hazijatajwa | 1000/= |
| 22. | Mafundi baiskeli | 1000/= |
| 23. | Bidhaa nyingine ambazo hazijatajwa | 1000/= |

SEHEMU YA SITA: ADA YA UKODISHAJI MITAMBO

| Namba. | Aina ya kifaa | Kiwango cha Ada kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Gari aina ya Isuzu Tipper lenye uwezo wa tani 10 | 2500/= kwa kila kilometa |
| 2. | Gari aina ya Isuzu Tipper lenye uwezo wa tani 7 | Isiyopungua 150,000/= |
| 3. | Lori la mizigo tani 3.5 na kreni | Isiyopungua 120,000/= |
| 4. | Mashine ya kuchanganyia saruji | 80,000/= |
| 5. | Mashine ya kutoa hewa kwenye sakafu | 50,000/= |
| 6 | Mfumo wa nafasi Kimataifa (GPS) | Kwa mujibu wa mkataba |
| 7 | Vifaa vya kufyatulia tofari | Kwa mujibu wa mkataba |

SEHEMU YA SABA: VIBALI VYA UJENZI

| Namba. | Aina ya ujenzi | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kiwanja cha makazi | 30,000/=kwa ujenzi wa nyumba moja na |

| | | |
|---|---|---|
| | | inayoongezeka italipiwa 20,000/= |
| | Makazi na Biashara | 50,000/= |
| 2. | Taasisi zisizo za serikali kwa nyumba ambazo sio ghorofa | 150,000/= |
| 3. | Kiwanda kikubwa | 300,000/= |
| 4. | Kiwanda cha uzalishaji | 150,000/= |
| 5. | Kiwanda kidogo | 150,000/= |
| 6. | Kituo cha mafuta | 330,000/= |
| 7. | Ukarabati | 15,000/= |
| 8. | Uzio<br>(a)Taasisi<br>(b)Binafsi | 1000/= kwa mita moja ya mzunguko.<br>1000/=kwa mita moja ya mzunguko. |
| 9. | Hifadhi ndogo,uwanja wa michezo,hoteli ya utalii ambayo sio ghorofa | 200,000/= |
| 10. | Ghorofa<br>Ghorofa 1-3 | 150,000/= |
| 11. | Ghorofa 4-6 | 200,000/= |
| 12. | Ghorofa 6 na kuendelea | 75,000/= kwa kila ghorofa inayoongezeka |
| 13. | Kuhuisha kibali cha ujenzi wa ghorofa | 75,000/= |
| 14. | Kusimika minara ya mawasiliano | 1,000,000/= |
| 15. | Kuhuisha kibali cha ujenzi usio ghorofa | Malipo yatakuwa sawa na yaliyolipwa |
| 16. | Mnara uliosimikwa eneo la mtu binafsi | 150,000/. |
| 17. | Ghala au bohari | 150,000/= |
| 18. | Kubadili matumizi ya Ardhi | 200,000/= |
| 19. | Sehemu ya kuoshea magari | 30,000/= kwa mwaka |
| 20. | Eneo la mapumziko | 100,000/= kwa mwaka |

## SEHEMU YA NANE: USHURU WA MAEGESHO YANAYOMILIKIWA NA HALMASHAURI

| Namba | Aina ya gari | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Gari lenye uwezo wa kubeba uzito wa tani 10 | 2500/= kwa siku |
| 2. | Lori lenye uwezo wa kubeba zaidi ya tani 10 | 3000/= kwa siku |
| 3. | Gari dogo | 1000/= kwa siku |
| 4. | Pikipiki ya magurudumu mawili | 500/= kwa siku |
| 5. | Pikipiki ya magurudumu matatu | 500/= kwa siku |

| | | |
|---|---|---|
| 6. | Gari dogo ya mizigo | 1500/= kwa siku |
| 7. | Ushuru wa kutunza gari lililokamatwa au kuzuiliwa | 20,000/= kwa siku |
| 8. | Ushuru wa kutunza pikipiki iliyokamatwa au kuzuiliwa | 10,000/= kwa siku |
| 9. | Guta | 500/= kwa siku |

SEHEMU YA TISA: USHURU WA STENDI

| Namba. | Aina ya chombo cha usafiri | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa | 3000/= kwa siku |
| 2. | Basi la kati | 2000/= kwa siku |
| 3. | Gari dogo la abiria | 500/= kwa siku |
| 4. | Gari dogo | 500/= kwa siku |
| 5. | Gari la mizigo:<br>lenye uwezo wa kubeba tani 1 hadi 3<br>lenye uwezo wa kubeba tani 4 hadi 10<br>lenye uwezo wa kubeba tani 11 na zaidi | 1000/= kwa siku<br>2000/= kwa siku<br>2000/= kwa siku |
| 6. | Pikipiki ya magurudumu matatu | 300/= kwa siku |
| 7. | Pikipiki ya magurudumu mawili | 200/= kwa siku |

SEHEMU YA KUMI: USHURU WA SOKO KWA MAZAO AU BIDHAA ZITOKAZO SOKONI

| Namba. | Aina ya Mazao au Bidhaa | kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 1000/= kwa kila gunia kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja |
| 2. | Maharage | 1500/= kwa kila gunia kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja |
| 3. | Muhogo | 500/= kwa kila gunia kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja |
| 4. | Mtama | 1500/= kwa kila gunia kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja |
| 5. | Mpunga | 1000/= kwa kila gunia kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja. |
| 6. | Dagaa | 3% ya bei ya dagaa ya siku husika |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Samaki na Mazao ya Samaki | 3% ya bei ya samaki ya siku husika. |
| 8. | Vitunguu | 1500/= kwa kila gunia kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja |
| 9. | Alizeti | 1000/= kwa kila gunia kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja |
| 10. | Kabeji au machungwa au miwa, nanasi au ndizi au parachichi | 7000/= kwa tani moja |
| 11. | Viazi | 1500/= kwa kila gunia kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja |
| 12. | Hoho | 500/= kwa tenga kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja |
| 13. | Karanga | 2500/= kwa kila gunia kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja |
| 14. | Njegere za maganda | 1000/= kwa kila gunia kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja |
| 15. | Pumba za mahindi | 500/= kwa kila gunia |
| 16. | Pumba za Mpunga | 500/= kwa kila gunia |
| 17. | Mashudu ya Alizeti | 1000/= kwa kila gunia |
| 18. | Nyanya | 500/= kwa kila tenga kwa mzigo wenye zaidi ya tani ya moja |
| 19. | Mchele | 2000/= kwa kila gunia kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja |
| 20. | Unga | 500/= kwa kila gunia kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja |
| 21. | Bidhaa nyingine ambazo hazijatajwa | 3,000/= kwa kila gunia kwa mzigo wenye zaidi ya tani moja |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA: ADA AU USHURU WA SHUGHULI ZA BURUDANI, UTAMADUNI, SANAA NA MATANGAZO

(Ada zote katika kipengele (1) - (7) zitalipwa kwa pamoja na mwenye sherehe)

| Namba. | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada au Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mshereheshaji | 20,000/= kwa tukio |
| 2. | Mpambaji wa kumbi za burudani | 20,000/= kwa tukio |
| 3. | Mmiliki wa kumbi | -ukumbi unaochukua watu 100 hadi 200 30,000/=kwa siku<br>-ukumbi unaochukua watu 300 hadi 500 50,000/= kwa siku |
| 4. | Matangazo ya barabarani ya sherehe | 40,000/= kwa tukio moja kwa siku |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | Mpishi wa chakula | 15,000/= kwa tukio moja kwa siku |
| 6. | Picha jongevu na mnato | 5,000/= kwa tukio moja kwa siku. |
| 7. | Matangazo ya kuuza bidhaa zinazopungua bei | 30,000/= kwa tangazo |
| 8. | Maombi ya kibali cha kufanya Tiba za Jadi | 30,000/= kwa siku |
| 9. | Tamasha | 100,000/= kwa tukio |
| 10. | Fete na bahati nasibu | 20,000/= kwa siku |
| 11. | Mnada (a) mali isiyohamishika<br>(b)mali nyinginezo | 1% ya kuuzia<br>40,000/= |
| 14. | Kupiga muziki ukumbi mkubwa | 30,000/= kwa siku |
| 15. | Kupiga muziki ukumbi mdogo | 30,000/= kwa siku |
| 16. | Matangazo ya biashara kwa kutumia vipaza sauti au vipeperushi au vitambaa na au fani za sanaa ambazo hazijatajwa hapo juu. | 30,000/= kwa siku. |
| 17. | Kumbi za picha mjongeo na mpira | -Ukumbi Mkubwa 30,000/= kwa mwezi<br>-Ukumbi wa Kati 20,000/= kwa mwezi<br>-Ukumbi Mdogo Mjini 15,000/= kwa mwezi<br>-Ukumbi Mdogo Vijijini 10,000/= kwa mwezi |
| 18. | Mashine ya bahati nasibu | 300,000/= kwa Mwaka |

SEHEMU YA KUMI NA MBILI: USHURU WA KULAZA VYOMBO VYA USAFIRI MAENEO YANAYOMILIKIWA NA HALMASHAURI

| Namba. | Aina ya chombo cha usafiri | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa | 3000/= kwa siku |
| 2. | Basi dogo | 2000/= kwa siku |
| 3. | Gari ndogo | 1000/= kwa siku |
| 4. | Gari dogo la mizigo | 1500/= kwa siku |

SEHEMU YA KUMI NA TATU: ADA YA USAJILI WA VYOMBO VYA USAFIRI

| Namba | aina ya gari | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Teksi | 50,000/= kwa Mwaka |
| 2. | Bajaji | 30,000/= kwa Mwaka |

SEHEMU YA KUMI NA NNE: USHURU WA MAZAO YA KILIMO

| Namba. | Aina ya Mazao | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mazao ya biashara | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia |
| 2. | Mazao ya chakula | Asilimia tatu (3%) ya bei ya kununulia. |

SEHEMU YA KUMI NA TANO: USHURU WA MAZAO YA MISITU

| Namba. | Aina ya Mazao | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Aina zote za mazao ya Misitu isipokuwa mitiki. | Asilimia tano (5%) ya bei ya kununulia |
| 2. | Mbao laini (saiplas au misindano) | 150/=kwa kila ubao |
| 3. | Mbao laini (mwembe,mnazi, Sederela) | 400/=kwa kila ubao |
| 4. | Mkaa gunia | 1000/=kwa kila gunia |
| 5. | Mbao za miti ya asili | 1,000/=kwa kila ubao |
| 6. | Kusafirisha mabanzi ya mitiki | (a)chini ya tani moja 10,000/=<br>(b)Tani 1hadi3--30,000/=<br>(c)Tani 4 hadi 7--40,000/=<br>(d) Zaidi ya Tani 7--45,000/= |
| 7. | Kusajili au kuchakata au kusafirisha biashara ya mazao ya Misitu | Asilimia 20 ya Tozo |
| 8. | Miti ya mitiki | 5,000/=kwa mita moja ya ujazo |
| 9. | Kusafirisha kuni | 5,000/=kwa tera |
| 10. | Asali | 200/=kwa kila lita |
| 11. | Nta | 200/=kwa kilo |
| 12. | Mianzi | 50/=kwa Mwanzi |

SEHEMU YA KUMI NA SITA: USHURU WA HUDUMA YA CHOO NA BAFU

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Choo | 200/= kwa huduma |
| 2. | Bafu | 300/= kwa huduma |

SEHEMU YA KUMI NA SABA: USHURU WA NYUMBA YA KULALA WAGENI

| Namba | Aina ya huduma | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa Nyumba ya Kulala | Asilimia 10 ya gharama anayolipa |

| | | |
|---|---|---|
| | Wageni | mgeni |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 15)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi .......................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MIMI MWENYEWE mbele ya.......................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba kwamba Tarehe ..........ya Mwezi .................. Mwaka................ nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya aya ya ……..ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba ya Mwaka 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri niko tayari kulipa kiasi cha shilingi………………………………………………………………………. badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.

Leo Tarehe ......................ya Mwezi ................................Mwaka ……

Jina: .....................................................

Saini: ....................................................

MBELE YA:

Jina……...............................................

Wadhifa: .................................................

Saini: .................................................

Tarehe: ...............................................

Lakiri la Halmashauri ya Mlimba imegongwa kwenye sheria Ndogo hii kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani Halmshauri ya Wilaya ya Mlimba uliofanyika Tarehe 27 Mwezi Oktoba Mwaka 2021 na Kushudiwa na Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya :-

ENG. STEPHANO B. KALIWA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba*

INNOCENT SIMON MWANGASA
*Mwenyekiti*

*Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba*

NAKUBALI,

Dodoma,
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*